6. Hali Ya Ushirika Kati Ya Polisi Na Uongozi Wa Serkali Pamoja Na Shirika Zisizo Za Serkali

Ushirika bora kati ya Polisi na Serkali chini ya uongozi wa waziri wa mambo ya ndani unapitia mwandishi mkuu ahusikaye na usalama wa Raia, pamoja na wakuu wa siasa na uongozi wa majimbo na mitaa yenye kujitegemea (entitées territoriales décentralisées)

Ripoti za ushirika kati ya askari polisi pamoja na jeshi, sheria na wizara zingine kupitia majadiliano ya kudumu.

7. Ushirika Mzuri Na Shurti Ya Kutumikia Raia

Kusimika tume za uchunguzi na zile za kuhakikisha uhuru na Usalama wa kazi.

Kuzidisha mikutano, mawasiliano na mazungumuzo kati ya Polisi na shrika la Raia.

Kutolea vituo vya upashaji habari na Shirika la Raia haki ya kutafuta habari kwa vituo vya Polisi, huku, siri za kikazi zikiheshimika.

Kusimika mipango ya kufuatilia mabadiliko haya yote

IV. KIFUNGO

Tangu sasa, Polisi haipashwi kuwa jeshi la kunyanyasa Raia ; bali kundi la watu wenye kutumikia Raia, lenye kupenda Inchi, wazalendo wasikiao oja za watu na kuheshimu viongozi wa Inchi, likiheshimu haki za binadamu pamoja na vyombo vya sheria ya Inchi, vya majimbo na vya kimataifa.

Hivyo, mabadiliko yanapitia mambo muhimu yafuatayo :

- Kuunda tume la kuhakikisha matumikio ya sheria
- Kudumisha uaminifu kati ya Polisi na Raia
- Mafundisho bora ya Uraia kwa wanainchi wote
- Kuzoeza polisi kuheshimu mipango ya kisiasa
- Kuchunguza na kufuatilia mabadiliko.

Shirika la Raia la Kongo linajihusisha kutumika pamoja na viongozi wa Inchi pia na Polisi (PNC) ili kubadilisha na kulifanya upya kundi la polisi ya Kongo na kufanya jitihada ili Raia ihishi ukweli wa mambo hayo yote.

MAWASILIANO

Kusini :

Joe Sanduku jossand2002@yahoo.com

Mashariki:

Loochi Kizungu, kloochi@yahoo.fr

Kinshasa:

Naupess Kibiswa: Socivilecd@yahoo.fr

Pst Madifuta Emery madifuta@yahoo.fr

Ferdinand Maholo maferdla@yahoo.fr

Maono haya yalisambazwa kwa watu wote na la Chaîne de Solidarité Agissante (Réseau des Commissions Justice et Paix des Confessions Religieuses) ikisaidiwa kikazi na kipesa na Idasa na DFID

SHIRIKA LA RAIA LA JAMUHURI YA KIDEMOKRASIA YA KONGO

MAKUNDI YENYE KUSHIKILIANA KWA KUTENDA KAZI

MAONO YA SHIRIKA LA RAIA KUHUSU POLISI MPYA YA KONGO

MSIMAMO WA KUBADILI NA KUFANYA UPYA POLISI YA KONGO (PNC)

I. KIINGILIO

Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ni inchi inayotoka katika vita vya miaka mingi, sasa inatarajia kudumisha sheria na haki katika ngazi zote za uongozi. Hivyo, tokea wakati wa ukoloni hadi leo, Raia wote wa Kongo wanaishi maisha ya kunyanyaswa na askari jeshi, askari polisi na hata ngazi za uongozi wa nchi.

Hali hiyo inafanya mawasiliano kati ya Polisi na Raia yawe yenye kukosa uaminifu tokea miaka mingi, popote inchini.

Hivyo, haja kubwa tena ya muhimu ya kurejesha mawasiliano bora kati ya Polisi na Raia wote wa Kongo, inajitokeza.

Kisha kutambua hali hiyo, Serkali ya Kongo imeanzisha mpango wa kubadilisha picha mbaya ya Polisi ya nchi. Na kwa upande mwengine, Shirika la Raia la Kongo limejihusisha na mabadiliko hayo, likitoa mapendekezo yake kwa viongozi wa nchi kuhusu doctrine mpya na maono mapya kwa Polisi mpya ya inchi yetu.

Katika kikartasi hiki, kundi « Chaine de Solidarité Agissante » linafikiri kutangaza maono hayo ya Polisi mpya ya Kongo.

II. HISTORIA NA MWENENDO WA MPANGO WA MABADILIKO YA POLISI

Mpango wa kubadilishwa Polisi ya inchi ya Kongo ulianzishia rasmi kutokana na barua yenye namba 25/cab/Min/Interdesec ya tarehe 14 novemba 2005, ilioyoandikwa na waziri wa mambo ya ndani, ambaye kwa tarehe hiyo aliunda kundi la mchangamano litakalo fikiri mambo kuhusu kubadilisha na kuunda Polisi mpya ya Kongo.

Kundi hilo lilijihusisha na:

- Kufanya uchunguzi dhidi ya Polisi (PNC) ya sasa
- Kuunda maoni (maombi) kuhusu hali na tabia za Polisi mpya katika kuheshimu katiba ya Inchi.
- Kutunga pendekezo la sheria kuhusu mwenendo na matumikio yake.

Kundi hilo lilitunga na kupeleka ripoti inayo husu pendekezo la sheria (loi organique) kwenye ofisi ya waziri na mambo ya ndani, kujitegemeza kwa majimbo na usalama, ili ikubaliwe kwanza na Serkali, kabla ya kuingizwa bungeni.

Hivyo ndivyo shirika la Raia lilishiriki katika mpango wa kuunda Polisi mpya inchini kwa msaada wa “Coopération Britanique”DFID, kupitia “Institut pour la Démocratie en Afrique”IDASA, na lilitoa mchango wake kuhusu maoni ya msingi ajili ya Polisi mpya ya Kongo.

III. MAONI YA MSINGI AJILI YA MAONO KUHUSU POLISI MPYA YA KONGO.

1. Doctrine

Polisi mpya inapashwa kuwa ya kiraia, moja, isiyo ya kisiasa, yenye kujua kazi, ikitumikia wanainchi wa Kongo katika haki na uongozi bora, huku ikiungana na Raia ambaye, ni kwa ajili yake ndio maana Polisi imeundwa.

2. Kazi

Polisi mpya inapashwa kuheshimu kanuni za sheria. Hivyo, inapashwa kujihusisha zaidi na kuelewa watu asili ya udemokrasia, sheria, haki za binadamu, jinsia na kumlinda mwanamke na mtoto kwa raia wote na kupiganisha utundu wa vijana, kuzagaa kwa watu wasio halali na kulinda mazingira.

3. Mapya

- Uraia na uzalendo wa Polisi, kutojihusisha na mambo ya siasa, kujihusisha zaidi kwa kuheshimisha haki za mtu pamoja na uhuru wake.
- Kuondoa Polisi katika hali yake ya uaskari kwa kufuta sheria zote zinazo ingiza Polisi kati ya askari jeshi, vikundi vyake na maadibisho yasifuate kanuni za kijeshi.
- Polisi katika kutenda kazi zake itastawishwa na services zingine zinazo kuwa na mamlaka kama vile (Polisi ya sheria ya mahakama na ofisi kuu ya mipakani ya DGM, Polisi ya RVA na ile ya ONATRA).

4. Usimamizi Wake

Kusimikwa kwa kamati kuu ya Polisi, Commissariat Général na Inspectorat Général ili kudumisha umoja katika kazi ya Polisi.

5. Mahifadhi Na Mali

I Mahifadhi ya kiutu

Polisi mpya inapashwa kuchunguza vizuri kwa kuheshimu umri, elimu na mwenendo wa mtu ili itimize kwa haki kazi zake.

II Fedha na vitu

Polisi mpya ya Kongo inapashwa kuwa na uwezo wa kutosha kipesa na kuwa na uhuru katika matumizi ya pesa hizo. Makazi yake na vifaa vya kazi vinapashwa kuwa na hali bora kwa kurahisisha Polisi kutimiza vema kazi zake.